Masuala ya Walaa na Baraa
Maana yake na Kuanza Kwake

Mtunzi

Prof. **Ibrahim Salah Al-Hud-hud**

Rais wa zamani wa Chuo Kikuu cha Al-Azhar

Kimetolewa na

Prof. **Muhammad Abdul Fadhil Al-Qusy**

Mjumbe wa Baraza kuu la Ulamaa
Makamu Mwenyekiti wa Taasisi

Kimefasiriwana

Ust. Muhammad Reda Abdelwahab

Ust. Ahmad Raafat Al-Sayed Mustafa

Kihakikiwa na

Ust. Fadhili Mansour

Kimepitiwa na

Dkt. **Sameh Anwar Bayoumi**

Jumuiya ya Kimataifa ya Wahitimu wa Al-Azhar

Mradi wa kupinga mitazamo mikali -

mfululizo wa kupinga mitazamo mikali (4)

Msimamizi Mkuu
Prof. **Muhammad Abdul Fadhil Al-Qusy**
Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Mradi
Usama Yasin
Mkurugenzi Mkuu wa Mradi
Hamdullah As-Safty
Namba ya usajili: 26643/2018
Namba ya Kimataifa: 978-977-85462-9-3

Tahadhari

Haki zote zimehifadhiwa na Jumuiya ya Kimataifa ya Wahitimu wa Al-Azhar Al-Sharif, hairuhusiwi kusambaza au kurudia kusambaza, au kutengeneza kitabu hiki au sehemu ya kitabu, au kukihifadhi kwenye vyombo vya uchapishaji pasi na kutangulia kuwepo makubaliano kwa maandishi na Jumuiya.

Jumuiya ya Kimataifa ya Wahitimu wa Al-Azhar

Mradi wa Kupinga Fikra za Misimamo Mikali

Chuo Kikuu cha Al-Azhar, Nasr City, Cairo, Arab Republic of Egypt

Namba ya Simu: +202 – 23868114

Fax: +202 23868116

Email: info@waag-azhar.org

Tovuti: www.waag-azhar.org

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema
Mwenye Kurehemu

Utangulizi

KWA UANDISHI WA PROF. MUHAMMAD ABDUL FADHIL AL- QUSY

MJUMBE KATIKA BARAZA KUU LA ULAMAA LA AL-AZHAR AL-SHARIF

Katika kitabu chake chenye utajiri wa maana na sura za kufikirika "Funguzi za Makkah" anasema Sheikh Mkuu "Muhyiddin Ibn Araby" kuwa: nafsi ya kweli ya Mwislamu: Haiwezekani kuwa hivyo pale yanaposimama makuzi yake ya nguvu ya ndani ya uelewa kwa kutoongezeka, basi ni lazima nafsi hiyo - katika mahusiano yake na ulimwengu pamoja na Muumba wa ulimwengu kupanda na kuongezeka kiroho kutoka hali ya kushuka kwa nguvu ya uelewa na kwenda kwenye hali nyengine iliyo juu zaidi, kinyume na hivyo nafsi hiyo itaendelea kuwa chini ya utawala wa mgando na kudumaa na kuwa rafiki wa usingizi na kifo!!

Kwa "Kupanda huku Kiroho" hukunjua peo zisizo na mwisho za nafsi ya mwanadamu, na viumbe vyote - kwa nafsi hiyo - vinakuwa vyenye uhai, huongea na Muumba wake pasi na ulimi, na kumsujudia bila ya mwili, pamoja na kuona ulimwengu kwa jicho la uzuri na upendo, roho na utulivu, hivyo humiliki kwa sifa hizo ulimwengu mzima na yaliyomo ndani yake yanayoonekana na yasiyoonekana.

Lau mtazamo huu wenye kuonekana ungechanganyika na sura ya Uislamu katika zama zetu za hivi sasa - basi ingekuwa ni kama kitendo cha uchawi katika utulivu wa nafsi yenye kiu ya haki na tumaini la usalama na uadilifu, ingekuwa ni tiba ya maradhi mengi ya zama na matatizo yake, na kugusa njia yake ya kwenda kwenye vifua na akili kuangazia nguvu ya giza na weusi wake usiochangayika na rangi nyingine!!

Lau mtazamo huu wenye kuonekana ungechanganyika na sura ya Uislamu katika zama zetu hizi, basi usingewakuta Waislamu isipokuwa ni watu vifua vyao vimekuwa na utulivu na huruma, wakisameheana msamaha mzuri, wakipata maumivu ya kuugua kwa wafiwa na maumivu ya wanyonge, na wakiwa juu ya vitimbi vya chuki na ubaya wa kinyongo na tabia mbovu, hawaoni kwa mwanadamu ndani ya zama zote isipokuwa nyoyo zikidondokea kwenye haki, na kupumzika kwa uzuri wa uadilifu na tamanio

la misingi bora pasi na matumizi ya nguvu yenye kuua, wala chuki mbaya, wala damu kumwagika au viungo kutawanyika au vichwa kukatwa!!

Lakini mtazamo huu mwepesi wenye kuonekana ambao unachanganyika na hisia za busara - kwa masikitiko - umebadilika katika zama zetu za sasa kutoka kinyume kwenda kinyume, bali kutoka utofauti kuwa tofauti… basi upo wapi huo mtazamo ndani ya taswira nyembamba ambayo watu wake wamehiyarishwa kuwa "Uislamu" kwa ujumla wake ukubwa wake na huruma zake umejisogeza na kujiingiza kwenye "Matamanio ya upendeleo binafsi wa mamlaka" na kujihusisha katika "Kujitumbukiza" kwenye usimamizi wa utawala, na Uislamu kwa - Watu hawa - umekuwa ni wenye kujikita na kujitenga kwenye "Mchezo wa Kisiasa" ambapo ni mazoezi na michezo, na kuondoka na mawimbi ya upepo peo zake na malengo yake makuu.

Upo wapi huo mtazamo kutokana na tabia zao mbaya ambazo zimepasua ulimwengu makundi mawili "Kundi" la imani ambayo haikimbiliwi isipokuwa na watu wa kundi hilo tu, na "Kundi" la ukafiri wa kijinga ambao hakuna jukwaa la kuuondoa na kumalizana nao, kisha watu wake - kwa mujibu wa mchezo wa kisiasa - wameanza kutembelea duniani kwa uharibifu na umwagaji damu, baada ya kuwaongoza vijana wengi wa Umma kwenye kuleta uadui na kuwaingiza kwenye shimo la kero, kisha wakawaacha wakipulizia moto wa vitendo vya nguvu na moto wa maangamizi, wakiwa na ari ya madaraka, na kukimbilia kwenye kiti cha mamlaka, na kuonja makazi ya utawala, kama kwamba hakuna kilichobakia katika "Uislamu" wote - roho maadili na misingi - isipokuwa ni "Mamlaka" yanayonyemelewa na "Utawala" wa kujipandisha, na "Uongozi" wenye kudharau roho za viumbe na kuruhusu kumwaga damu.

Upo wapi huo mtazamo kutokana na hao ambao wanajinasibisha na "Usalafi" na kudai kuwa ndio warithi wake, kisha wanaufanya kuwa ni sitara ya udanganyifu pindi wanapojumuishwa kwenye utasa wa kifikra pamoja na chuki na mitazamo ya upande mmoja, mpaka wakaingiza umuhimu wa Waislamu katika maumbile yaliyoingizwa kutoka nje, na mandhari ambazo zimefungua mlango - ulioegemewa baada ya hapo - na walinganiaji ugaidi, hapa ninamaanisha kile kinachoitwa katika fika zao zenye kuzunguka "Vita vya kundi lenye kuzuiliwa", wazo ambalo linakaribia kuwa shari yenye kujikita kimakubaliano na makundi mengi ya matumizi ya nguvu hapo zamani na hata hivi sasa.

Upo wapi huo mtazamo kutokana na makundi ya kigaidi yenye majina ya chuki ambayo yamekuwepo ndani ya zama zetu hizi yakijiingiza kwenye udanganyifu na uzushi kwa jina la Uislamu na utawala wa Kiislamu, kisha walinganiaji wake hufanya uharibifu duniani kwa vitendo vya mauaji na

mateso, pamoja na kukata shingo za watu mbele ya jicho la ulimwengu, pasi na kufumba jicho wala kugonga mioyo yao, bali pasi na kujitokeza kwa watu wao walioganda kifikra kuona kiwango cha uhalifu ambao wameusukumia kwenye haki ya Uislamu pale walipokutanisha sura yake na sura ya umwagaji damu bali pindi walipoubadilisha “Uislamu” kwa athari za vitendo vyao hivi - katika mtazamo wa wengi - kuwa ni janga lenye kupiga ulimwengu mzima, na nini kinakuwa katika “Sura ya Kiakili” ambayo imejikita kwenye kumbukumbu za “Watoto Ulimwenguni” kuhusu “Uislamu” ambao wanadai kuulingania na kuinua bendera yake pamoja na kuinua neno lake?

Kisha hawa watu na hao hawaangalii kuwa matokeo ya “Jihadi ya Kiroho” ya Kiislamu katika mwelekeo tofauti yanapaswa kumuinua binadamu kwenye peo za juu kiroho, kiakili na kwa nguvu za ufahamu, yanayomhamasisha mwanadamu kwenye kuimarisha matunda yake kwa wenye njaa walio uchi na wagonjwa, kuimarisha tonge la kuishi na kiwango cha dawa, kunyoosha maisha na kumsukuma kwenye kumaliza ubinafsi mbaya ambao ni zao la ustaarabu wa manufaa ya vitu?

Huenda katika mfululizo huu wa kielimu tunajaribu kurudisha haki sehemu yake, na kufafanua kile kilichobandikwa na watu hao kwenye Uislamu ikiwa ni miongoni mwa mambo yanayoleta shaka na kusababisha makosa, ili kuwaonesha vijana ukweli wa Uislamu, na yanayopaswa kuwa nayo katika mwelekeo wao kwenye kupata radhi za Mola wao na kumfuata Mtume wao S.A.W.

Mwenyezi Mungu tunamuomba uwezesho na kukubali, Yeye ndiye Mbora wa kuombwa na kwake ni kwenye matumaini yote.

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu

Utangulizi

Hakika mahubiri ya chuki na mafundisho yake hayawezi kusimamisha jamii ya wanadamu inayofunikwa na huruma pamoja na kuhurumiana, ni katika jambo lisilowezekana Mtume S.A.W. ambaye ametumwa na Mola wake kuwa ni rehema kwa walimwengu kuwa mlinganiaji wa chuki, bughudha na uadui.

Qurani Tukufu imetanga hilo kwa uwazi katika kauli yake Mola Mtukufu: ﴿**Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote**﴾{Anbiyaa, 107}.

Aya haikumvua na kumwacha yeyote ya kuwa Mtume S.A.W. ni rehema kwa walimwengu wote kuanzia wanadamu, majini, wanyama, ndege na viumbe vyengine, hivyo Ujumbe wa Uislamu umekuwa ni Ujumbe wa ulimwengu, kwani Mola Amemwambia Mtume wake S.A.W. Akisema: ﴿**Na usemi wake Mtume ni: Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika hawa ni watu wasioamini ۞ Basi wasamehe, na uwaambie maneno ya amani. Watakuja jua**﴾{Az-Zukhruf, 88: 89}.

Pamoja na kuwa wao si wenye kuamini lakini Mtume S.A.W. aliamrishwa kuwasamehe, na kuongea nao maneno mazuri.

Na sisi kwenye kitabu hiki tutafuata njia ya watu wasomi ya kuonesha kwanza rai tofauti na dalili zake, kisha tutaleta majibu yake kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, hivyo ndiyo njia ya Mtume S.A.W. katika kusahihisha uelewa. Masahaba walikuwa kwanza wanaulizwa na Mtume S.A.W. ili kufahamu maana ya neno kisha anafanya kazi ya kulirekebisha.

Mfano wa hayo ni kauli yake kwa Masahaba: “Je! Mnamfahamu ni nani mtu mwenye kufilisika?” wakasema: Mtu mwenye kufilisika ni yule ambaye hana pesa ya Dirham wala Dinar wala vitu, akasema Mtume S.A.W.: “*Mtu mwenye kufilisika katika Umma wangu ni yule atakayekuja Siku ya Kiyama akiwa na ibada zake za Sala, Funga na Zaka, lakini anakuja akiwa amemtukana huyu, amemsingizia huyu, amekula mali ya huyu, amemwaga damu ya huyu na amempiga huyu, anapewa huyu katika mema yake na huyu kwenye mema yake, ikiwa mema yake yatakwisha kabla ya kulipa yale yaliyo juu yake, basi huchukuliwa makosa yao na kutupiwa yeye kisha anatupiwa Motoni*”[(1)].

(1) Hadithi imepokelewa na Imamu Muslim katika Sahihi yake kwenye Kitabu cha Wema na Kuunganisha Udugu, mlango wa Uharamu wa Dhuluma.

Maana ya Walaa na Baraa kwa Wanaoizungumzia[1]

Walaa: Ni kumpenda Mwenyezi Mungu, Mtume wake pamoja na Masahaba na Waumini wenye kumpwekesha Mwenyezi Mungu na kuwatetea.

Baraa: Ni kumchukia mwenye kwenda kinyume na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Masahaba na Waumini wenye kumpwekesha Mwenyezi Mungu, miongoni mwa washirikina, wanafiki na wazushi na wafanya maasi.

Nafasi ya Walaa na Baraa kwao

Nafasi ya Imani ya *Walaa* na *Baraa* katika Sharia ni kubwa na ni nguzo miongoni mwa nguzo za Imani, na miongoni mwa ukubwa wa nafasi hii:

Kwanza: Ni sehemu katika maana ya Shahada, nayo ni kusema "Hapana Mola" katika tamko la "Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu" Maana yake ni kuepukana na kila kinachoabudiwa kinyume na Mwenyezi Mungu.

Pili: Ni sharti katika Imani, kama Alivyosema Mwenyezi Mungu: ﴿**Utawaona wengi wao wanafanya urafiki na waliokufuru. Hakika ni maovu yaliyotangulizwa na nafsi zao hata Mwenyezi Mungu Amewakasirikia, nao watadumu katika adhabu ۞ Na lau wangelikuwa wanamuamini Mwenyezi Mungu, na huyu Nabii, na yaliyoteremshwa kwake, wasingeliwafanya hao marafiki. Lakini wengi katika wao ni wapotofu**﴾{Al-Maidah, 80: 81}.

Tatu: Imani hii ndiyo kishikizo kinachotegemewa zaidi katika Imani kwa Hadithi aliyoipokea Ahmad katika Kitabu chake kutoka kwa Al-Baraa Ibn Azib *Mwenyezi Mugu R.A.* amesema: amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu S.A.W.: "*Kishikizo kinachotegemewa zaidi katika Imani ni kupenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kuchukia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu*" Katika Hadithi Sahihi: "*Mwenye kupenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kuchukia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na akatoa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na akazuia kutoa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, basi hakika imekamilika Imani yake*" Imepokewa na Abou Daud.

---

(1) Huu ni mtazamo wa watu wa zamani wa Al-Khawarij, na kufuatiwa na Ibn Taimiya na Muhammad Ibn Abdulwahhab pamoja na Abdulaziz Ibn Baz na Saleh Al-Uthaimin pamoja na Salim Al-Qahtaniy, na kurejewa katika kitabu cha mjumuiko wa kitabu cha Fatawa za Ibn Taimiya, na kitabu cha mjumuiko wa Fatawa za Ibn Al-Uthaimin, pamoja na kitabu cha Fatawa za Ibn Baz.

Nne: Ni sababu ya kuonja utamu wa Imani na ladha ya yakini, kwa Hadithi iliyotoka kwa Mtume S.A.W. amesema: "*Mambo matatu mwenye kuyapata, amepata utamu wa Imani: Kuwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake ni vipenzi vyake kuliko wengine, na kumpenda mtu hampendi isipokuwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na kuchukia kurudi kwenye ukafiri kama anavyochukia kutupwa motoni*" Hadithi hii imekubaliwa na Wanachuoni wote wa Hadithi.

Tano: Ni kiunganishi ambacho husimama kwacho jamii ya Kiislamu ﴿**Hakika waumini wote ni ndugu**﴾{Al-Hujraat, 10}.

Sita: Kwa kufikiwa Imani hii unapata ukaribu wa Mwenyezi Mungu, kwa Hadithi iliyopokelewa na Ibn Abbas *Mwenyezi Mungu awe radhi nao* amesema: "*Mwenye kupenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na akachukia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na akafanya urafiki kwa ajili ya Mwenyezi Mungu akafanya uadui kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, basi hakika atapata ukaribu wa Mwenyezi Mungu kwa hilo*".

Saba: Ni kuwa kutofikiwa Imani hii kunaweza kupelekea kuingia kwenye ukafiri, Amesema Mwenyezi Mungu: ﴿**Na mwenye kufanya urafiki nao miongoni mwenu basi naye ni katika wao**﴾{Al-Maidah, 51}.

Nane: Kupokelewa kwake kwa wingi ndani ya Qurani na Hadithi kunajulisha juu ya umuhimu wake.

Miongoni mwa kauli za Mashekhe wao

Anasema Shekhe Hamad Ibn Atiq R.A.: "Ama kuwafanyia uadui makafiri na washirikina jua kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu Amewajibisha hilo na Amesisitiza wajibu wa hilo, na Ameharamisha kuwafanya marafiki na Akasisitiza katika hilo mpaka imekuwa hakuna katika Qurani hukumu yenye dalili nyingi na zilizo wazi kuliko hukumu hii baada ya kuwajibisha Tawheed na kuharamisha kinyume chake".

Amesema Shekhe Al-Islam Ibn Taimiya: "Hakika kufikiwa kwa shahada ya kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu, kunahitaji kutopenda isipokuwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kutochukia isipokuwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wala kutofanya urafiki isipokuwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wala kutofanya uadui isipokuwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na kupenda Apendacho Mwenyezi Mungu , na kuchuki Achukiacho Mwenyezi Mungu" na akasema pia: "Mwenye kuamini kuwa Makanisa ni nyumba za Mwenyezi Mungu, na kwamba Mwenyezi Mungu Anaabudiwa humo, na wanayoyafanya Mayahudi na Wakristo ni Ibada ya Mwenyezi Mungu na taa ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, au kwamba yeye anapenda hilo na analiridhia au aliwasaidia kuyafungua na kusimamisha

Dini yao, na kufanya hivyo ni lengo la kujiweka karibu na Mwenyezi Mungu au ni utiifu, basi huyo ni kafiri". Na akasema pia katika sehemu nyingine: "Mwenye kuamini kwamba kuwatembelea watu wa dhimma kwenye Makanisa yao ni kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu, basi huyo ameritadi".

Miongoni mwa Sura za Kuwafanya Makafiri Marafiki kwao ni

1. Kujifananisha nao katika mavazi na maneno.
2. Kuishi katika miji yao, na kutohama miji yao na kwenda miji ya Kiislamu kwa ajili ya kukimbia Dini.
3. Kusafiri kwenye miji yao kwa ajili ya matembezi na kustarehesha nafsi.
4. Kuwafanya kuwa ni wasiri na washauri.
5. Kufuata kalenda zao hasa kalenda ambayo inaelezea ibada zao na sikukuu zao, kama kalenda ya kuzaliwa Yesu.
6. Kujiita majina yao.
7. Kushiriki katika sikukuu zao au kuwasaidia katika kusherehekea au kuwapongeza kwa mnasaba wake au kuhudhuria sherehe zake.
8. Kuwasifu na kusifu walivyo navyo katika teknolojia na staarabu, na kupendezewa na tabia zao na vipaji vyao pasi na kuangalia Imani zao batili na dini yao ya uharibifu.
9. Kuwaombea msamaha kwa Mwenyezi Mungu na kuwatakia rehema.

Dalili zao kwenye Qurani Tukufu

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

1. ﴿**Hakika nyinyi mna mfano mzuri kwenu kwa Ibrahim na wale waliokuwa pamoja naye, walipowaambia watu wao: Hakika sisi tumejitenga nanyi na hayo mnayoyaabudu badala ya Mwenyezi Mungu. Tunakukataeni na umekwisha dhihiri uadui na chuki baina yetu**﴾{Al-Mumtahina, 4}.

2. ﴿**Na ni tangazo kutokana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa wote siku ya Hija Kubwa kwamba Mwenyezi Mungu na Mtume wake hawana jukumu lolote kwa washirikina**﴾{Al-Tawbah, 4}.

3. ﴿**Enyi mlioamini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa ni marafiki. Wao ni marafiki wao kwa wao. Na miongoni mwenu mwenye kufanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wenye kudhulumu. Utawaona wale wenye maradhi**

nyoyoni mwao wanakimbilia kwao wakisema: Tuna hofu yasitusibu mabadiliko. Huenda Mwenyezi Mungu Akaleta ushindi au jambo jingine litokalo kwake wakawa wenye kujuta kwa waliyoyaficha katika nafsi zao﴾{Al-Maidah, 51:52}.

4. ﴿**Enyi mlioamini! Msiwafanye adui zangu na adui zenu kuwa marafiki mkiwapa mapenzi**﴾{Al-Mumthina,01}.

5. ﴿**Waumini wasiwafanye makafiri kuwa wapenzi wao badala ya Waumini. Na anayefanya hivyo, basi hatakuwa chochote mbele ya Mwenyezi Mungu. Ila ikiwa kwa ajili ya kujilinda na shari zao. Na Mwenyezi Mungu Anakuhadharisheni naye**﴾{Aal-Imraan, 208}.

6. ﴿**Enyi mlioamini! Msiwafanye wasiri wenu watu wasiokuwa katika nyinyi. Hawataacha kukufanyieni ubaya. Wanayapenda yanayokudhuruni. Imekwisha fichuka chuki yao katika midomo yao. Na yanayoficha vifua vyao ni makubwa zaidi**﴾{Aal-Imraan, 118}.

7. ﴿**Enyi mlioamini! Msiwafanye baba zenu na ndugu zenu kuwa vipenzi vyenu ikiwa wanapenda ukafiri kuliko Imani. Na katika nyinyi atakayewafanya hao ndio vipenzi vyake, basi hao ndio madhalimu**﴾{Al-Tawbah, 23}. Ni wazi kuwa katazo ni lenye vigezo na wala silo katazo la moja kwa moja.

8. ﴿**Huwakuti watu wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho kuwa wanawapenda wanaompinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hata wakiwa ni baba zao, au watoto wao, au ndugu zao, au jamaa zao. Hao ameandika katika nyoyo zao Imani, na amewapa nguvu kwa Roho itokayo kwake. Na atawaingiza katika Mabustani yapitayo mito kati yake. Humo watakaa daima. Mwenyezi Mungu awe radhi nao, na wao wawe radhi naye. Hao ndio kundi la Mwenyezi Mungu. Hakika Kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kufanikiwa**﴾{Al- mujaadalah, 22}.

Ni wazi kabisa kwa mwenye macho kwamba kukataza kumefunganishwa na kumpinga Mwenyezi Mungu na kuwafanyia uadui, na wala si kukataza moja kwa moja.

Mtazamo wa ajabu

Hawa watu wametofautisha kati ya Walaa na Baraa na kati ya utaifa, kwani utaifa ni aina ya mashirikiano ya kidunia, ama Walaa na Baraa kinachokusudiwa hapo ni kuwapenda Mawalii wa Mwenyezi Mungu na kuwachukia maadui wa Mwenyezi Mungu, wewe unaishi nao maisha ya kidunia lakini moyoni mwako huwapendi bali unawachukia, na hili halikuzuii kushirikiana nao kwa wema, kama Alivyosema Mwenyezi Mungu:

﴿**Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na ucha-Mungu**﴾{Al-Maidah, 8}.

Maelezo: Ni wazi kabisa katika yaliyotangulia kwamba wao wanatoa ushahidi kwa Maandiko pasi na kuangalia mfano wake katika Qurani Tukufu na vilevile katika Hadithi Tukufu, na hilo ni ufahamu mbaya wa Andiko Takatifu, kama inavyoonesha kwa uwazi kuwa wanazusha katika Dini uzushi ambao haukuzungumziwa na waja wema waliotangulia, jambo ambalo linawafanya kuharakisha kuwakufurisha wasioamini imani yao mbovu, na hili linatengeneza hatari kubwa kwa Waislamu wenyewe na binadamu kwa ujumla.

Maana Sahihi ya Kadhia hii

Kwanza: Hakuna yeyote katika waja wema waliotangulia wala Maimamu wanne aliyezingatia Walaa na Baraa kuwa ni katika nguzo za Imani wala nguzo za Uislamu, na Wanazuoni wote wa Umma wamekubaliana kwamba nguzo za Imani na Uislamu ni zile zilizokuja katika Hadithi Sahihi: Kutoka kwa Umar Ibn Al-Khattab R.A. Amesema: “Tulipokuwa kwa Mtume S.A.W. siku moja, akatokea mtu mwenye nguo nyeupe mno, nywele nyeusi mno, hana athari ya safari wala hakuna yeyote kati yetu anayemjua, mpaka akakaa mbele ya Mtume S.A.W. akaegemeza magoti yake juu magoti yake na akaweka viganja vyake juu mapaja yake na akasema: Ewe Muhammad nieleze kuhusu Uislamu? akasema Mtume S.A.W.: "*Uislamu ni kushuhudia kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu na Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, kusimamisha Sala, kutoa Zaka, kufunga mwezi wa Ramadhani na kuhiji nyumba ya Mwenyezi Mungu ukiwa na uwezo wa kwenda*". Akasema: umesema kweli. Tukamshangaa anauliza na anasadikisha! Akasema: Nieleze kuhusu Imani? Akasema Mtume: "*Ni kumuamini Mwenyezi Mungu na Malaika wake, Vitabu vyake, Mitume yake na kuamni Siku ya Mwisho kuwa ipo pamoja na kuamini kadari Kheri yake na Shari yake*". Akasema: umesema kweli. Akasema nieleze kuhusu wema? Mtume Akasema: "*Ni kumuabudu Mwenyezi Mungu kama kwamba unamuona ikiwa wewe humuoni basi yeye anakuona*". Akasema: Nieleze kuhusu Kiyama? Akasema: "*Hakuwa mwenye kuulizwa mjuzi zaidi kuliko mwenye kuuliza*" akasema: Nieleze dalili zake? Akasema Mtume: **"***Mjakazi kumzaa bwana wake, utawaona watu wanatembea peku wakiwa uchi, masikini wachunga mbuzi, wanajenga majumba marefu marefu!*" Kisha akaondoka, Mtume akasubri kidogo kisha akasema: "*Ewe Umar unamjua aliyeuliza*" nikasema: Mwenyezi Mungu na Mtume wake ni wajuzi zaidi. Akasema: "*Hakika yule ni Jibril amewajia kuwafundisha Dini*

yenu[1]" Hadithi hii ipo wazi kabisa katika kuziainisha na kuzibainisha nguzo za Uislamu na nguzo za Imani.

Amesema Abu Al-Hassan Al-Ash'ary: "Imani ni kusadikisha kwa moyo, ama kusema kwa ulimi na kuzifanyia kazi nguzo ni matawi yake, basi mwenye kusadikisha kwa moyo, kwa maana akakiri upweke wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, akakiri Mitume kwa kusadikisha waliyokuja nayo kutoka kwa Mwenyezi Mungu, basi imesihi Imani yake, hata akifa sasa hivi na Imani hiyo, atakuwa Muumini aliyeokoka, wala hatoki katika Imani isipokuwa kwa kukanusha kitu katika hivyo. Na amesema Al-Baqalaniy: "Na kujua kwamba kumuamini Mwenyezi Mungu ni kusadikisha kwa moyo" hivyo basi hakuna katika Elimu ya Tawheed kinachoitwa Walaa na Baraa, kwani ni katika matendo ya moyoni ambayo yanatokana na athari ya Imani, na mandhari ya kimaadili ya Walaa ni utetezi na uungaji mkono, na mandhari kimaadili ya Baraa ni kufanya uadui na kutounga mkono, na hudhihirika mandhari ya Walaa na Baraa kimsingi ni katika matendo ya moyoni, ambayo yanatokana na athari za Imani, hakika Muumini ambaye amemuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake pamoja na Vitabu vyake, Malaika wake, Siku ya Mwisho na Kadari, Kheri yake na Shari yake Imani hii huotesha katika moyo wake mapenzi na ukaribu na kuwanusuru Waumini wote kwa haki, pia huotesha katika moyo wake kuepukana na Imani na fikra ambazo zinapingana na anayoyaamini. Na mandhari ya kitabia katika Walaa ni kutetea na kuunga mkono, na mandhari ya kitabia katika Barraa ni kufanya uadui na kutounga mkono, na yanadhihirika mandhari ya Walaa na Barraa pale anapoamua anayepinga Imani yako na utambulisho wako kukudhulumu na kuipiga vita nchi yako, hakika Walaa inahitaji kusimama na nchi yako, watu wako, na utambulisho wako, na kuepukana na adui ambaye anataka kubomoa utambulisho wako, usalama wako na taifa lako.

Hivyo basi, hakika Walaa na Baraa ni lazima viwepo daima katika mfumo wa maisha ya Mwislamu pamoja na asiye kuwa Mwislamu, kunapasa kwa Mwislamu kujitegemeza kwenye Uislamu na kulinda utambulisho wake wa Kiislamu pasi na kuharibu misingi ya kuishi pamoja kwa amani na watu na hii ndiyo Walaa, na Baraa ni kulinda Mwislamu kutochanganya Imani yake na ambacho kinaweza kuitia mashaka na mfano wake pasi na kuingia katika kukufurisha au kuifanyia Uadui nafsi iliyolindwa.

Hakika kutowapenda wasiokuwa Waislamu katika raia na wengineo ambao hawapo katika vita na Waislmu kwa maana kuwafanyia uadui watu wao na kuwaudhi, kunakwenda kinyume na Maandiko ya Qurani na Hadithi.

---

(1) Hadithi imepokelewa na Imamu Muslim kwenye Sahihi yake, Kitabu cha Imani, mlango wa Ubainishaji wa Uislamu na Imani.

Mwislamu ameamrishwa kusema kwa wema na watu wote pasi na kubagua. Mwenyezi Mungu Anasema: ﴿**Na semeni na watu kwa wema**﴾{Al-Baqarah, 83} na Akasema Mwenyezi Mungu: {**Hakika Mwenyezi Mungu Anaamrisha kufanya uadilifu, na hisani**﴾{Al-Nahli, 90}. Mwenyezi Mungu hakutukataza kuwafanyia wema wasiokuwa Waislamu, kuungana nao, kuwapelekea zawadi, kukubali zawadi kutoka kwao na mengine miongoni mwa kuwafanyia wema. Mwenyezi Mungu Amesema: ﴿**Mwenyezi Mungu hakukatazeni kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu**﴾{Al-Mumtahinah, 8}.

Tatizo ni ufahamu wa Imani kwa wanaojiita watu wa Salaf kuwa ni: kusadikisha kwa moyo na kutamka kwa ulimi na kufanya matendo kwa viungo na nguzo, inazidi kwa utiifu na inapungua kwa maasi. Mwenyezi Mungu Amesema: ﴿**Na wazidi Imani wale walioamini**﴾{Al-Muddathir, 31}.

Na hapa ndipo walipomkufurisha kila mwenye kufanya maasi, na asili yao ni Al-khawarij.

Pili: **Maana sahihi ya Aya mbili za uhimili wa Imani na nyenginezo:**

Aya ya Kwanza: Ni neno lake Mwenyezi Mungu: ﴿**Enyi mlioamini! Msiwafanye adui zangu na adui zenu kuwa marafiki mkiwapa mapenzi, na hali wao wamekwisha ikataa haki iliyo kujieni, wakamfukuza Mtume na nyinyi kwa sababu mnamuamini Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wenu**﴾{Al-Mumtahinah, 01}.

Hapana budi kutoa muongozo sababu ya kushuka kwa Aya hii. Aya hii imeshuka kwa Sahaba Hatib Ibn Abi Balta'a, aliandika ujumbe wa siri na kuwapelekea maadui wa Makkah anaweleza kuwa Mtume S.A.W. anajiandaa kuwapiga vita, na Mwenyezi Mungu Akamuelezea Mtume S.A.W. jambo hilo, wakamkamata mwanamke aliyebeba ujumbe huo kwa watu wa Makkah maadui wa Mtume S.A.W. na maadui wa dola ya Kiislamu, ikashuka Aya inayoharamisha kuwafanya marafiki maadui, hili ni jambo la kawaida hawezi yeyote kulipinga, kwa sababu linaendana na tabia ya mwanadamu, mahusiano ya watu ya kawaida wenyewe kwa wenyewe na kwa mataifa yote mpaka zama zetu hizi, hakika mwenye kumfanya rafiki adui wakati wa vita na anatoa siri za vita anafanya kosa kubwa la jinai, na ili kufahamu sahihi ambako hakuharibu sababu ya kushuka kwa Aya hii wala Hadithi wala Andiko jengine, imekuja sababu ya kushuka ambayo tumeilezea kwa ufupi katika vitabu vyote vya Wanazuoni wa Tafasiri ya Qurani na Vitabu vya Hadithi Sahihi [1].

(1) Angalia katika sababu ya kushuka kwenye Kitabu cha Imamu Bukhari Hadithi ya 3007, na Kitabu cha Imamu Muslim Hadithi namba 2494, na Abu Daud

Aya ya Pili: ﴿**Enyi mlioamini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa ni marafiki. Wao ni marafiki wao kwa wao. Na miongoni mwenu mwenye kufanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wenye kudhulumu. Utawaona wale wenye maradhi nyoyoni mwao wanakimbilia kwao wakisema: Tunahofu yasitusibu mabadiliko. Huenda Mwenyezi Mungu Akaleta ushindi au jambo jingine litokalo kwake wakawa wenye kujuta kwa waliyo yaficha katika nafsi zao**﴾{Al-Maidah, 51, 52}.

Aya imeshuka kwa Abi Libabah na akasema Al-Suddy: Imeshuka Aya hii siku ya Uhud Waislamu walipoogopa mpaka baadhi yao walitaka kuwafanya marafiki Mayahudi na Wakristo, na kauli nyengine: Aya hii imeshuka kwa Ubadah Ibn Al-Samit na Abdullah Ibn Ubay Ibn Salul, Ubadah akajiweka mbali na kuwafanya Mayahudi marafiki na kuwa nao karibu, Ibn Ubay akaendelea kushikamana nao na akasema: Mimi naogopa kugeuka kibao(1).

Na inabainika hilo kuwa Aya imeshuka katika vita, na ni jambo la kawaida kuwa haifai kutaka msaada kwa maadui na kuwafanya marafiki wakati wa vita, wala si hoja kwetu kwa kusema: Mazingatio ni ujumla wa tamko na wala si umaalumu wa sababu, kwa sababu sisi tunasema, kwa maana ya Aya ni kutofaa kuwafanya marafiki wakati wa vita, kwa Aya zitakazokuja baadaye ambazo zinalingania kuwafanyia wema na uadilifu muda wa kutokuwa na vita kati yetu na wao.

Aya ya Tatu: ﴿Enyi mlioamini! Msiwafanye wasiri wenu watu wasiokuwa katika nyinyi. Hawataacha kukufanyieni ubaya. Wanayapenda yanayokudhuruni. Imekwisha fichuka chuki yao katika midomo yao. Na yanayoficha vifua vyao ni makubwa zaidi﴾{Aal- Imraan, 118}.

Aya yenyewe ina majibu tosha, kwa hakika imekusanya sababu ya kukataza kumfanya rafiki anayedhamiria uadui, na anakusudia Waumini kupatwa na madhara. ﴿**Hawataacha kukufanyieni ubaya**﴾ kwa maana: Wanafanya juhudii kubwa ili mharibikiwe ﴿**Wanayapenda yanayokudhuruni. Imekwisha fichuka chuki yao...** ﴾ kwa maana: Wanatamani mpatwe ma matatizo na kuwazidishia uzito na wametangaza hilo, na kutangaza kwao ni kidogo sana kuliko wanachoficha ndani ya nyoyo zao, kukataza hapa ni kuna vigezo na wala si kukataza tu moja kwa moja, na

---

Hadithi namba 2650, na Imamu Tirmidhy Hadithi namba 3305, na Imamu An-Nisaai Hadithi namba 11521, na Imamu Ahmad katika Kitabu chake Hadithi namba 600, na sababu ya kuchuka kwenye Kitabu cha Imamu Wahidiy Hadithi namba 448 – 449, na Tafasiri ya Imamu Qurtubiy 20/ 396.

(1) Kitabu cha Al-Jaami'i cha Hukumu za Qurani cha Imamu Qutubiy, 8/45.

kanuni inaacha sharti kwenye hali yake na kuacha amri huru kwenye uhuru wake.

Aya ya Nne: ﴿Waumini wasiwafanye makafiri kuwa wapenzi wao badala ya Waumini. Na anayefanya hivyo, basi hatakuwa chochote mbele ya Mwenyezi Mungu. Ila ikiwa kwa ajili ya kujilinda na shari zao. Na Mwenyezi Mungu Anakuhadharisheni naye﴾{Aal- Imraan, 20}.

Katazo la hapa pia ni katazo lenye kigezo au sharti, kwa maana: Haifai kumfanya rafiki asiyekuwa Mwislamu hali ya kuwepo Mwislamu ambaye anafaa kuwa rafiki.

Tatu: Haifai kuelewa Aya hizi mbali na Aya zengine, kinyume na hivyo Qurani itakuwa inajigonga. Aya nyingi zimetutaka kumfanyia wema mpinzani na kushirikiana naye vizuri, kwa sababu hiyo ulinganiaji wa Kiislamu umejikita katika usamehevu na huruma, na huu ni ushahidi wa hilo:

Hakika Uislamu umelingania wema kwa wanadamu isipokuwa waliotudhihirishia uadui. Mwenyezi Mungu Amesema: **﴿Mwenyezi Mungu hakukatazeni kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu﴾**{Al-Mumtahinah, 8}.

Qurani imebainisha kuwa Mtume S.A.W. amekuja na amani na si vita, na kuwa uti wa mgongo wa Ujumbe wa Uislamu ni huruma kwa binadamu wote, hilo lipo wazi katika kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu Akimsifu Mtume wake na kubainisha malengo ya Ujumbe wake: **﴿Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote﴾**{Al-Abiyaa, 107}.

Hakika Uislamu unaweza kupambana na ukatili na itikadi kali, kwani Uislamu unajali amani kwa ujumla na unalingania kujadiliana na watu wa Vitabu "Mayahudi na Wakristo kwa wema". Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: **﴿Wala msijadiliane na Watu wa Kitabu ila kwa njia iliyo nzuri kabisa﴾**{Al-A'nkabuut, 46}.

Pia Uislamu unalingania kutoamsha chuki na mifundo. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: **﴿Wala msiwatukane hao wanaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu, wasije na wao wakamtukana Mwenyezi Mungu kwa jeuri bila ya kujua﴾**{Al-An'aam, 108}.

Pia unalingania ujirani mwema na kuacha kuanzisha shari. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: **﴿Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu﴾**{Al-Maidah, 8}.

Hakika misingi ya Uislamu inaamini uwepo wa staarabu nyingi na unakiri, na hilo linathibitisha Imani katika nyoyo za Waislamu, na mwenendo

mzuri wa Mtume wa Mwenyezi Mungu na Sahaba zake Watukufu, umeelezea Imani kwa uwepo wa staarabu nyingi na tamaduni tofauti, na umeishi nazo kawaida na “Kukusanyika staarabu ni ishara miongoni mwa ishara za historia ya staarabu za kibinadamu, nayo ni kadari isiyoshindika au kuepukika, na daima kwa mujibu wa kanuni hii inayohukumu kumetimia kupambanua kati ya vitu ambavyo wanashirikiana binadamu wote na vitu maalumu kwa staarabu". Na chaguo mbadala la mgongano wa staarabu ni kubadilishana staarabu za kibinadamu ili mwanadamu apate kheri na faida, na kuelekea kutengeneza mwitiko wa staarabu kwa ajili ya changamoto zilizopo, kinyume na nadharia ya “Mgongano wa Staarabu” ambao unasukuma upande uliopo wenye silaha kwa uwezo wa kivitendo na kifedha, kutawala na kupinga wengine na kushikilia uwezo wake na utajiri wake kwa madai ya kuwa migogoro ya ulimwengu ujao itatawala upande wa staarabu. Hakika misingi ya Kiislamu inathibitisha katika nyoyo za Waislamu kwamba "Kujitenga na kujifunga mwenyewe katika ulimwengu wa leo ambao umegeuka kuwa kijiji kidogo kwa hukumu ya maendeleo ya kiufundi makubwa katika teknolojia ya mawasiliano ni jambo lisilowezekana, kama vile kufuata ulinganiaji wa staarabu moja duniani pia ni kuuthibitisha utawala wa staarabu wa kikatili, nayo ni njia ya kufuata staarabu ambayo kila Umma utakosa staarabu yake maalum na kutaibadilisha kuwa uwanja wa staarabu katili" .

Uislamu umesisitiza kwa wafuasi wake kwamba uwingi na mgawanyiko ni katika mwenendo wa Mwenyezi Mungu Aliouweka katika ulimwengu wake, na kwamba madhumuni ya Ujumbe wake ni kutowalazimisha watu kwenye dini moja, wingi ni mwenendo miongoni mwa mienendo Aliyoiweka Mwenyezi Mungu ulimwenguni. Amesema Mwenyzi Mungu Mtukufu: ﴿**Kila mmoja katika nyinyi Tumemwekea sharia yake na njia yake**﴾{Al-Maidah, 48}.

Na Akasema tena: ﴿**Na Mola wako Mlezi Angelipenda Angewafanya watu wote wakawa Umma mmoja. Lakini hawaachi kutofautiana, Isipokuwa wale ambao Mola wako Mlezi Amewarehemu, na kwa hiyo ndio Mwenyezi Mungu Amewaumba**﴾{Hud, 118: 119}.

Na Akasema: ﴿**Hapana kulazimisha katika Dini. Kwani Uongofu umekwisha pambanuka na upotofu**﴾{Al-Baqarah, 256}.

Akasema tena: ﴿**Basi kumbusha! Hakika wewe ni Mkumbushaji. Wewe si mwenye kuwatawala**﴾{Al-Ghashiya, 21: 22}.

Hakika misingi ya Uislamu haifanyi uadui kwa Dini zilizotoka mbinguni, na Qurani imeelezea kwamba kuamini Mitume na Vitabu vivyoteremshwa ni sharti katika ukamilifu wa Imani ya Mwislamu, katika neno lake Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Mtume ameamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa**

Mola Mlezi wake, na Waumini vile vile. Wote wamemuamini Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na Vitabu vyake na Mitume wake. Hatutafautishi baina ya yeyote katika Mitume wake﴾{Al-Baqarah, 285}.

"Pia haifai kueleweka huu usamehevu wa kibinadamu ambao umewekwa na Uislamu kuwa ni msingi madhubuti wa kusimika mahusiano ya Mwislamu na asiyekuwa Mwislamu kuwa ni mpasuko au maandalizi ya kuyayusha ndani ya nchi yoyote ambayo haikubaliani na madhumuni ya Dini hii, usamehevu huu hauondoi tofauti na hitilafu, lakini unatengeneza mahusiano ya kibinadamu ambayo Uislamu unataka yaongoze maisha ya watu, hivyo kusisitiza mambo maalumu ya Kiimani, staarabu na tamaduni, hakuna njia ya kuondoa, lakini Uislamu hautaki kwenye haya mambo maalumu kuzuia muingiliano wa Kiistaarabu kati ya Mataifa na raia na kusaidiana wao kwa wao".

Hakika ulinganiaji wa Kiislamu umetilia mkazo juu ya utofauti wa watu na jamii, hakuna njia ya mawasiliano isipokuwa kwa kujuana na kushirikiana, na imekuja katika hilo kauli ya Mwenyezi Mungu: ﴿**Enyi watu! Hakika Sisi Tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na Tumekufanyeni kuwa mataifa na makabila ili mjuane**﴾{Al-Hujraat, 13}.

Hakika ulinganiaji wa Kiislamu unatilia mkazo usamehevu na mazungumzo na wala si migongano, kuishi kwa pamoja si kuuwana, na yamekuja Maandiko ya Qurani na Hadithi Tukufu zikibainisha hilo kwa wazi. Mwenyezi Mungu Amemuamrisha Mtume wake kusamehe wasiokuwa Wauamini. Mwenyezi Mungu Amesema: ﴿**Na usemi wake Mtume ni Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika hawa ni watu wasio amini. Basi wasamehe, na uwaambie maneno ya Amani. Watakuja jua**﴾{Az-Zukhruf, 88: 89}. Pia Amemuamrisha kusamehe kuliko kuzuru ﴿**Basi samehe msamaha mzuri**﴾{Al-Hijri, 85}. Na Anasema Mwenyezi Mungu: ﴿**Shikamana na kusamehe, na amrisha mema, na jitenge na wajinga**﴾{Al-A'araf, 199}. Na neno lake Mwenyezi Mungu: ﴿**Waambie walioamini wawasamehe wale wasiozitaraji siku za Mwenyezi Mungu, ili awalipe kwa waliyokuwa wakiyachuma**﴾{Al-Jaathiya, 14}.

Na si katika malengo ya Uislamu wala katika Ujumbe wake kuwafanya Waislamu wasiokuwa Waislamu, bali lengo lake kusherehesha uhakika wa Uislamu, na kwamba nafasi yake ni kulinda usafi wa Sharia ya Kiislamu na kuitetea.

Na kwamba Uislamu haubebi chuki kwa Imani nyengine, Uislamu unalaani ukatili na ugaidi, hakika watu wote wameumbwa na Mwenyezi Mungu kutokana na nafsi moja, na kutofautiana katika Imani ni katika tabia ya binadamu, na Imani haziuzwi wala hazinunuliwi, wala hakuna

kulazimishana katika Imani, na kwamba hitilafu hazizuii kushirikiana wala kujuana.

Hakika misingi ya Kiislamu inatulingania sote kujenga amani kati ya binadamu wote, hakika vitu vinavyowakusanya binadamu ni vingi, basi tufaidike navyo katika kusimamisha umwagaji damu, tushirikiane sote katika kuzitakasa hisia za kidini kutokana na chuki na mifundo ambayo imemgharimu mwanadamu thamani kubwa na ya kuchosha, basi tuungane sote enyi watu ili kukabiliana na ukatili, njaa na umasikini, na tushirikiane sote ili kumfurahisha wanadamu.

Ninawashukuru nyote

Amani iwe kwenu na rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka zake

Yaliyomo

Utangulizi 3
Utangulizi 6
Maana ya Walaa na Baraa 7
kwa Wanaoizungumzia 7
Nafasi ya Walaa na Baraa kwao 7
Miongoni mwa kauli za Mashekhe wao 8
Miongoni mwa Sura za Kuwafanya Makafiri Marafiki kwao ni 9
Dalili zao kwenye Qurani Tukufu 9
Mtazamo wa ajabu 10
Maana Sahihi ya Kadhia hii 11

مشيخة الأزهر

مركز الأزهر للترجمة

Al-Azhar Center for Translation (ACT)